

# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

Simu: +255 22-2928468  
Fax: +255 22-2928469  
Barua pepe: info@kigamboni.go.tz  
Tovuti: www.kigambonimc.go.tz



S.L.P. 36009,  
KIGAMBONI,  
DAR ES SALAAM,  
TANZANIA.

## TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI NDUGU STEPHEN KATEMBA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA KIGAMBONI YA KWAMBA MNATAKIWA KUOMBA KIBALI CHA UJENZI KABLA YA KUFANYA MAENDELEZO YOYOTE KATIKA VIWANJA/MAJENGO MNAYOMILIKI, VIWE VYA KUPIMWA AU AMBAVYO HAVIJAPIMWA.

AGIZO HILI NI KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA SHERIA 124 NA 125 VYA KANUNI ZA KISHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA MIJI) (UDHIBITI UENDELEZAJI),SURA 128 GN 242 YA MWAKA 2008, AMBAYO INAELEKEZA UJENZI WOWOTE NDANI YA MAMLAKA ZA UPANGAJI AMBAZO NI MAMALAKA ZA MIJI MIDOGO, HALMASHAURI ZA MIJI, MANISPAA NA MAJIJI NI LAZIMA UPATE KIBALI CHA UJENZI KUTOKA KWENYE MAMLAKA HUSIKA.

FAIDA ZA KIBALI CHA UJENZI NI PAMOJA NA MPANGILIO MZURI WA MIJI,KURAHISISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA JAMII, KUEPUKA MIGOGORO ISIYO YA LAZIMA NA KUEPUKA HASARA INAYOWEZA KUTOKEA PINDI JENGO LINALOJENGWA BILA KIBALI.

### **UKIUKWAJI WA AGIZO HILI UTAPELEKEA:**

1. KULIPA FAINI KWA MUJIBU WA SHERIA, TARATIBU NA KANUNI.
2. KUBOMOLEWA KWA JENGO LILIOJENGWA BILA KIBALI.
3. KUFIKISHWA MAHAKAMANI NA KUSHTAKIWA KWA KOSA LA KUJENGA BILA KIBALI.

KWA MAELEZO ZAIDI FIKA KATIKA OFISI YA MHANDISI WA MANISPAA ILIYOPO KARIBU NA KITUOCHA AFYA KIGAMBONI MKABALA NA KITUO CHA POLISI KIGAMBONI ILI UPATE UTARATIBU WA KUPATA KIBALI CHA UJENZI KWA MUJIBU WA MUONGOZO WA UTOAJI VIBALI VYA UJENZI NA USIMAMIZI WA UJENZI WA MAJENGO KWENYE MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

**IMETOLEWA NA :**

**KITENGO CHA TEKNOLOJIA HABARI NA MAWASILIANO  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**28/06/2018.**